



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA RAIS KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

SERA YA USAFIRI WA WATUMISHI WA UMMA

SEPTEMBER, 2014



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA RAIS KAZI NA UTUMISHI WA UMMA

SERA YA USAFIRI WA WATUMISHI WA UMMA

SEPTEMBER, 2014

YALIYOMO

YALIYOMO.....	i
TAFSIRI YA MANENO MUHIMU.....	v
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 HALI YA USAFIRI KATIKA UTUMISHI WA UMMA.....	3
2.1 Usafiri wa Nchi kavu.....	3
2.2 Usafiri wa Baharini.....	4
2.3 Usafiri wa Anga.....	4
3.0 HAJA YA SERA YA USAFIRI.....	5
3.1 Haja ya Sera ya Usafiri.....	5
4.0 DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA.....	6
4.1 Dira ya Sera.....	6
4.2 Dhamira ya Sera.....	6
4.3 Lengo Kuu la Sera.....	6
4.4 Malengo Mahsusi ya Sera.....	6
4.5 Malengo, Hoja, Matamko na Mikakati ya Sera.....	7
4.5.1 Lengo la Sera 1: Kuweka mfumo mzuri wa upatikanaji na ugawaji wa vyombo vya usafiri kwa taasisi na watendaji.....	7
4.5.2 Lengo la Sera 2: Kuwapatia watumishi wa Umma Posho za usafiri wa kwenda na kurudi kazini	9
4.5.3 Lengo la Sera 3: Kuweka utaratibu wa kutumia vyombo vya usafiri vya sekta binafsi katika usafirishaji wa watumishi wa Umma na wageni maalum katika shughuli za Serikali	10
4.5.4 Lengo la Sera 4: Kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mikopo ya vyombo vya usafiri.....	12
4.5.6 Lengo la Sera 5: Kuweka muundo wa Kitaasisi na	

Muongozo wa Kisheria wa Usimamizi wa huduma za usafiri wa watumishi wa umma	13
4.5.6 Lengo la Sera: Kusimamia matumizi na matangenezo ya vyombo vya Serikali	14
4.5.7 Lengo la Sera 7: Kuweka taratibu nzuri za safari za watumishi wa Umma ndani na nje ya nchi.....	16
4.5.8 Lengo la Sera 8: Kuhakikisha kuwepo kwa mfumo mzuri wa uwekaji wa takwimu za vyombo vya usafiri na safari za watumishi wa Umma.....	17
5.0 WADAU WA SERA YA USAFIRI YA WATUMISHI WA UMMA NA MAJUKUMU YAO.....	18
5.1 Serikali Kuu.....	18
5.2 Wizara inayohusika na Usafiri.....	18
5.3 Wizara inayoshughulikia Utumishi.....	19
5.4 Wizara inayoshughulikia masuala ya fedha....	19
5.5 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.....	19
5.6 Sekta Binafsi.....	20
5.7 Makundi ya kijamii na wananchi.....	20
5.8 Vyombo vya Habari.....	20
5.9 Washirika wa Maendeleo.....	20
6.0 UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI YA SERA	21
6.1 Vyombo vya Utekelezaji.....	21
6.2 Ufuatiliaji na Tathimini ya Sera.....	21
6.3 Utaratibu wa Kupitia na Kurekebisha Sera....	22


DIBAJI

Huduma ya usafiri katika utumishi wa umma ni miongoni mwa nyenzo muhimu inayomuwezesha Mtumishi kutekeleza majukumu aliyopangiwa kwa ufanisi ndani na nje ya Nchi. Kwa kuzingatia ukweli kwamba watumishi wa Umma wanaishi katika, Miji, Mikoa, Wilaya, Shehia na Mitaa tofauti hivyo hulazimika kutumia usafiri ili kuwawezesha kufika katika vituo vyao vya kazi (Ofisini) na kurejea katika makaazi yao. Watumishi huhitaji usafiri ambao unawawezesha katika kufuatilia utendaji wa majukumu yao yenye kutekeleza Dira ya 2020, Malengo ya Millenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA).

Kufuatiakuwepo kwamalalamiko mengi ya watumishi kuchelewa kufika kazini kwa wakati, kutokuwepo kwa utaratibu mzuri wa usimamizi wa Usafiri kwa Watumishi na kuzorota kwa shughuli za utendaji katika Serikali kunakohusishwa na matatizo ya usafiri wenye kukidhi mahitaji. Hivyo basi ni muhimu kuwepo kwa Sera ya usafiri kwa Watumishi wa Umma ambayo itahakikisha kwamba Watumishi wa Serikali katika ngazi zote wanapatiwa huduma ya usafiri wenye uhakika.

Serikali kupitia Ofisi inayosimamia masuala ya Utumishi na Wizara inayosimamia Miundo mbinu na Mawasiliano imeamua kuanzisha Sera ya Usafiri wa watumishi wa umma itakayotoa muelekeo kwa Watumishi wa Umma katika kupatiwa huduma ya usafiri. Aidha, Sera imeweka wazi msimamo wa Serikali wa kuunga mkono masuala ya kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa Watumishi wote.

Katika kuandaa Sera hii wadau mbalimbali wameshirikishwa ambao wameweza kutoa mchango mkubwa uliopelekea kukamilika kwa Sera ambayo matarajio yangu ni kwamba yataimarisha huduma za utawala na utendaji Serikalini na kuchochea hisia za uwajibikaji na hatimae kuwa na utumishi wenye tija kwa Taifa.



.....
MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma

